مفهوم العبادة

# MAANA YA IBADA

**Hotuba ya Kwanza.**

**Imefasiriwa na profesa.**

**Ayman Al-asar**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitakatifu: {**Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na Mola wenu basi muabuduni hii ndio njia iliyonyooka**} ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mola peleka sala na salamu pamoja na baraka kwake pia na kwa watu wake na Maswahaba zake na wale waliomfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi**:

Ibada ina sehemu tukufu na nafasi ya juu kabisa, yenyewe ndio lengo kubwa ambalo kwa ajili yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba viumbe, ambapo Anasema Mola wa haki Utukufu ni wake: {**Si kuumba majini wala wanadamu isipokuwa lengo wafanye ibada**} pia Anasema: {**Hatukupeleka Mtume kabla yako isipokuwa tulimfunulia ufunuo kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa Mimi basi abuduni**}.

Ibada ndio kazi kubwa ya mwanadamu katika maisha yake yote, kwani anasema Hassan Al-Baswary *Mungu amrehemu*: Hakika Mwenyezi Mungu hajayapa muda matendo ya Muumini bila ya kifo.

Mwenye kuzingatia Sharia ya Kiislamu atakuta kuwa maana ya Ibada ni aina mbili, aina ya kwanza: Ni pana sana inakusanya milango yote ya kheiri, kama vile kufanya kazi za kutafuta riziki, maadili mema, ukweli katika mazungumzo, usamehevu kwa mwenye kukosea, kufanya mazuri kwa watu, kuhudumia familia na mengine katika matendo mema, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Hakuna kheiri nyingi katika maongezi yenu isipokuwa ni kwa mwenye kuamrisha utoaji**

**wa sadaka au mema au kufanya mambo mazuri kwa watu na mwenye kufanya hayo kwa kutegemea radhi za Mwenyezi Mungu basi tutampa malipo makubwa**}, na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: "*Kila salamu inayotolewa kwa watu kwa kila siku inayochomozewa na jua ni sadaka, kufanya uadilifu kati ya watu wawili ni sadaka, mtu kusaidiwa kwa mnyama wake akambeba au kumbebea vitu vyake ni sadaka, neno zuri ni sadaka, kila hatua anayoikata kuelekea kwenye Ibada ya sala ni sadaka, kuondoa adha na kero njiani ni sadaka*".

Kama vile kuijenga ardhi kupitia kazi za kilimo, uzalishaji wa viwanda, kufanya kazi kwa umahiri mkubwa inayopelekea mafanikio kwa jamii nzima na kuwa ni sababu ya ustawi wa nchi na maendeleo yake ni katika Ibada ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu anazipenda sana, nazo ni zenye kutakiwa sana na Mola Mtukufu ambapo Anasema: {**Yeye ndiye aliyekuwekeni nyinyi kwenye ardhi na kuwajengeeni humo**}, na anasema Mtume wetu S.A.W: "*Mtu mwenye kupendwa sana na Mwenyezi Mungu ni yule mwenye manufaa zaidi kwa watu, na matendo yenye kupendwa zaidi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni furaha kuingiza kwa Muislamu, kwa kumuondolea matatizo, au kumlipia deni au kumuondolea njaa, na kuyaendea mahitaji ya ndugu yangu ni jambo nilipendalo sana kuliko kukaa itikafu ndani ya Misikiti huu mwezi mzima – kwa maana ya – Msikiti wa Madina, na mwenye kumtatulia tatizo ndugu yake basi Mwenyezi Mungu atazithibitisha nyayo zake siku ya kudondoka nyayo*".

Na maana ya pili ya Ibada ni maana maalum, ikiwa inakusanya uendelezaji wa alama za Uislamu, kutekeleza nguzo za swala, zaka, funga, hija ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Tekelezeni Ibada za swala na swala ya katikati na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu**} na Anasema tena Mola Mtukufu: {**Enye mlio amini mumelazimishwa kutekeleza Ibada ya funga kama walivyolazimishwa ambao wamewatangulia ili mpate kumcha Mungu**} na Anasema pia Mola Mtukufu: {**Na endelezeni Ibada ya swala na mutoe zaka na kile munachokitanguliza katika mambo ya kheir basi mutakikuta kwa Mwenyezi Mungu**} na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Na amri ya Mwenyezi Mungu kwa watu ni kutekeleza Ibada ya hija kwa mwenye uwezo, na mwenye kupinga basi Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosheleza kwa viumbe**}.

**Hotuba ya Pili:**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, sala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho *rehma na amani ziwe kwake* pamoja na Watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Tunasisitiza kuwa mtu aliyesawa ni mwenye kuleta uwiano kati ya utekelezaji wa amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu ikiwa pamoja na Ibada za swala funga zaka hija kwa mwenye uwezo wa kuielekea Ibada hiyo, na katika kazi za kuujenga ulimwengu na kujipamba na maadili mema.

Kama vile tunasisitiza kuwa Ibada kwa maana yake maalum haileti mafanikio yake isipokuwa pale inapo athiri maadili na tabia za mwanadamu, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Hakika ya Ibada ya swala hukataza maovu na machafu**} na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: "*Siku ambayo mmoja wenu amefunga basi asiongee maneno machafu, ikiwa atatukanwa na yeyote au kumpiga basi na aseme: Mimi nimefunga*", na anasema tena Mtume S.A.W "*Hakika yangu nimeletwa ili kukamilisha maadili mema*", mwenye kukuzidi kwenye maadili mema basi amekuzidi kwenye ufahamu sahihi wa dini.

**Ewe Mwenyezi Mungu tuwezeshe kukutaja Wewe na kukushukuru pamoja na kutekeleza vyema Ibada zako.**